*Ruaha Catholic University, Journal of Education and Development (RUCUJED), Volume 3, Issue 1, 2024*

# Mchango wa Matumizi ya TEHAMA katika Ufundishaji wa Stadi ya Kusoma kwa Wasambaa Wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya Pili

Davian Buguna
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Barua pepe: davianjames24@gmail.com

**Ikisiri**

*Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha yanaendelea kushamiri kote duniani. Ukuaji wa teknolojia unasaidia kurahisisha na kuchagiza uelewa wa wajifunzaji katika stadi mbalimbali za lugha. Makala haya yalilenga kudodosa maoni ya walimu wa Kiswahili kama lugha ya pili wilayani Lushoto, kuhusu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa Wasambaa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Data za makala haya zimekusanywa kwa njia ya usahili. Nadharia iliyotumika kuongoza utafiti huu ni modeli ya Ukubalifu wa Teknolojia ya Devis (1989). Watoataarifa waliotumika ni walimu kumi (10) kutoka katika shule tano (5) za msingi wilayani Lushoto mkoani wa Tanga. Mkabala wa kitaamuli umetumika katika uchanganuzi wa data. Matokeo yanaonesha kuwa matumizi ya TEHAMA yamekuwa na mchango mkubwa katika kurahisisha na kuboresha mbinu za kitamaduni za ufundishaji wa stadi ya kusoma na wale wasiotumia TEHAMA wanaona kuwa matumizi ya TEHAMA katika mazingira ya vijijini yana changamoto nyingi za kimazingira, kiujuzi na kiuchumi ambazo hukwamisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma.*

**Manenomsingi**: Matumizi ya TEHAMA, ufundishaji, stadi ya kusoma.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yalilenga kuchunguza mchango wa TEHAMA[1] katika ufundishaji stadi ya kusoma kwa Wasambaa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili (Lg2) nchini Tanzania. Ili kufikia lengo kuu hilo makala haya yalikuwa na lengo mahususi moja la kudodosa mawazo ya walimu wa Kiswahili kuhusu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa Wasambaa wanaojifunza Kiswahili kama Lg2.

Maendeleo ya TEHAMA yamedhihirisha mabadiliko mengi chanya katika taaluma nyingi, ikiwa ni pamoja na ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2 au lugha ya kigeni. Mabadiliko mengi yamefanyika katika mifumo ya elimu, mihutasari ya masomo kutokana na ukubalifu wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Padurean (2009) anaeleza kuwa matumzi ya TEHAMA hususani kompyuta katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2 yamepangwa

[1] TEHAMA ni kifupi cha "Teknolojia ya Habari na Mawasiliano". Maneno haya yana maana ya jumla inayorejelea mifumo yote ya kiteknolojia inayotumika kutengeneza, kuhifadhi, kuchakata, na kutumia habari.

katika madarajia kadhaa kulingana na majukumu yake katika darasa. Madarajia hayo ni kama vile: daraja la mwalimu, daraja la ujaribizi (upimaji), daraja la nyenzo, daraja la kiwezishi cha mawasilianao (communication facilitator), na daraja la chanzo cha data.

Darajia la TEHAMA kama mwalimu uhusisha matumizi ya programu ya 'CD ROM' katika ufundishaji na ujifunzaji. Programu hii humwezesha mwanafunzi kusikiliza vipindi mbalimbali vilivyorekodiwa, kutazama video mbalimbali, kuongea kupitia vipazasauti, kujifunza maneno kwa kubofya katika picha kisha kusikiliza matamshi sahihi ya jina la picha husika. Hata hivyo, maendeleo ya TEHAMA yanaendelea kuibua mbinu mpya zaidi katika darajia hili kama vile matumizi ya wavuti, ambayo ni mbadala wa programu ya 'CD ROM' kwani humwezesha mwalimu kushiriki kwa kuweka mawazo au nukuu zake mwenyewe, hivyo kuboresha ufundishaji.

Pia, darajia la TEHAMA kama kijaribizi (nyenzo ya upimaji) huwawezesha wajifunzaji katika kujipima kiwango cha ujuzi walichokifikia katika stadi yoyote ile ya lugha wanayojifunza. Wanafunzi hutumia progamu za kimtandao zinazotoa mazoezi mbalimbali ambayo huwa yametengenezwa na kuwekewa mipaka ya kimatumizi. Pia, matumizi ya TEHAMA kutimiza lengo hili hukabiliwa na changamoto ya kuwa na majibu ya NDIO au HAPANA kwa kiwango kikubwa. Hivyo, matumizi hayo humpunguzia mjifunzaji Lg2 kupata maelekezo ya kutosha kuhusu usahihi wa majibu yanayotakiwa.

Aidha, darajia la TEHAMA kama chanzo cha data/taarifa ni jambo ambalo aghalabu kila mmoja anaweza kuwa analifahamu vizuri, kuwa kupitia TEHAMA na mfumo wa mtandao unaweza kupata data zozote unazozitaka. Jambo muhimu ni kuwa walimu wanapaswa kuwapatia wanafunzi wao kurasa maalumu kulingana na maarifa ya stadi husika wanayohitaji wanafunzi hao kuyapata. Jambo hili litasaidia kuwaondolea wanafunzi hali ya kutembelea kurasa nyingi ambazo hazina msaada kwao katika ujifunzaji wa Lg2.

Vilevile, darajia la TEHAMA kama kiwezeshi cha mawasiliano hutumika kuwawezesha wanafunzi kuwasiliana na wenzao kupitia mkutano kwa njia ya video au sauti na barua pepe n.k. Mwalimu huweza kuandaa mijadala ya vikundi vidogovidogo vya wanafunzi wa sehemu tofauti tofauti kwa njia hii ya TEHAMA. Matumizi haya ya TEHAMA huchochea uwezo wa wanafunzi kuwasiliana na kuimarisha stadi mbalimbali za lugha.

Aidha, Hermans, Tondeur, Van-Braak, na Valcke (2008) wameainisha hatua tatu za kuzingatiwa zinazohusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji Lg2 ambazo zinaonekana pia kuafikiwa na walimu. Wanaeleza kuwa hatua hizo ni uhusishaji, uwezeshaji, na usaidizi. Uhusishaji ni utekelezaji wa matumizi sahihi ya TEHAMA katika mada husika, kwa kuhusisha upatikanaji wa uelewa wa dhana ngumu na ujuzi utakaowezesha mafanikio ya mwanafunzi, ilhali uwezeshaji huhusisha matumizi ya TEHAMA katika ukaziaji wa maarifa ya mada iliyotambulishwa. Mathalani matumizi ya powerpoint huwezesha kuwasilisha mada kwa njia ya ubunifu unaosababisha kuibua mijadala, na kushiriki mawazo na fikra mbalimbali. Kuhusu usaidizi, matumizi ya TEHAMA yanatazamwa kama zana na msaada wa kimaarifa unaowawezesha wanafunzi kujifunza. Wanafunzi katika hatua hii huitumia TEHAMA kutafuta nukuu mbalimbali za kuwasaidia kukamilisha kazi zao, kutuma kazi kupitia barua pepe kwenda kwa walimu wao na hata kuwawezesha kuwa wenye upangilifu na bora katika kufanya kazi zao. Uanishaji huu umejumuisha kwa pamoja baadhi ya vipengele ambavyo Padurean (2009) ameviweka katika madarajia tofauti. Hata hivyo, ubora na udhaifu wa uanishaji huo si sehemu ya mjadala wa makala haya. Kimsingi, Makala haya yanalenga kuchunguza kwa ujumla matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa madarasa ya awali, na Kiswahili kikiwa Lg2.

Ni dhahiri kuwa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2 yana umuhimu mkubwa ukiachilia mbali ni kwa namna gani yanatumika. Altun (2015) anaunga mkono mawazo haya kwa kupendekeza kuwa uhusishaji wa teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji huchochea utayari wa ujifunzaji hali inayorahisisha kufikiwa kwa lengo la ujifunzaji. Hivyo basi ni muhimu kwa walimu wa lugha kuhakikisha wanakuwa na ujuzi mpana wa TEHAMA na kuutumia darasani ili kuweza kufikia malengo ya wajifunzaji (Instefjord & Munthe, 2017; Proshkin, Glushak, & Mazur, 2018). Ufundishaji wa kisasa unahitaji kuhusisha mbinu za kisasa na zile za kitamaduni kulingana na mazingira husika.

Vilevile bin Noordan na Yunus (2022) wanaeleza kuwa uhusishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma umechangia katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi, kuchochea ushiriki wao wakati katika mchakato wa ujifunzaji na kuboresha mtazamo wao juu ya kupenda lugha wanayojifunza. Pia, Akintunde na Angulu (2015) wanaeleza kuwa suala la matumizi ya

TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji haliwezi kupuuzwa hasa katika zama hizi za teknolojia. Matumizi ya TEHAMA yamedhihirika kwa muda mrefu sasa kuwa ni muhimu katika mchakato wa ujifunzaji wa stadi mbalimbali za lugha. Aidha, walibaini kuwa baadhi ya changamoto za kutumia Teknolojia katika nchi zinazoendelea katika ufundishaji na ujifunzaji ni uchumi mdogo wa kuweza kumudu kununua na kuendesha vifaa hivyo katika mazingira ya shule hali hiyo ina ambatana na uhaba wa umeme katika maeneo ya vijijini na changamoto za mtandao. Hata hivyo ongezeko la matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji katika maeneo mengi ya nchi hizi yanaonesha matokeo chanya kwa watumiaji wake. Hivyo makala haya, yanadodosa mtazamo wa walimu wa Kiswahili kwa kuzingatia mchango wa TEHAMA katika ufundishaji stadi ya kusoma kwa wanafunzi wa madarasa ya awali wilayani Lushoto.

**2.0 Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu umeongozwa na kiunzi cha nadharia kilichopendekezwa na Davis (1989) cha Ukubalifu wa Teknolojia. Kiunzi cha Ukubalifu wa Teknolojia kinaundwa na vipengele viwili vya msingi ambavyo ni kutazamwa kwa urahisi wa kutumiwa na kutazamwa kuwa wenye manufaa. Davis (1989) anadai kwamba ugumu wa kutumia mfumo wa habari unaweza kuondoa manufaa na faida za mfumo huo, na pia kuathiri kukubalika na kuridhika kwa mtumiaji. Kutazamwa kwa urahisi wa kutumiwa inafupishwa na kujulikana kama KUUKU hufafanuliwa kama “kiwango ambacho mtu anaamini kwamba kutumia mfumo fulani kutamwondolea matumizi ya nguvu.” Ikiwa watumiaji wanaona matumizi ya mfumo wa habari kuwa muhimu kusaidia utendakazi wao wa sasa na wa muda mrefu wa kazi, kuna uwezekano mkubwa wa kutumia mfumo huo katika utendaji wao wa kila siku. Aidha, kutazamwa kuwa wenye manufaa inafupishwa na kujulikana kama KUWEMA hufafanuliwa kama “kiwango ambacho mtu anaamini kwamba kutumia mfumo fulani kungeongeza utendaji wake wa kazi (wa sasa na unaoendelea)”. Hivyo basi, misingi hiyo miwili ya nadharia imetumika katika kutuongoza kudodosa mtazamo wa walimu kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa Kiswahili ikiwa ni Lg2 kwa Wasambaa.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu umefanyika wilayani Lushoto. Sampuli ya walimu kumi (10) waliopatikana kwa mbinu ya usampulishaji kusudio ndio walitumika kama watoataarifa. Watoataarifa waliokusudiwa katika utafiti huu ni walimu wanaofundisha Kiswahili darasa la kwanza na la pili. Walimu hao wameteuliwa katika shule tano za msingi ambazo ni Malindi juu, Malindi chini, Muhelo, Nzigha, na Mtindili. Shule zilizoteuliwa zilitumika kuwakilisha shule nyingine zote wilayani Lushoto kwa kuwa zote wanafunzi wanajifunza Kiswahili kama Lg2. Aidha, wilaya ya lushoto iliteuliwa kwa kuwa huaminika kuwa wazungumzaji asilia wa lugha ya Kisambaa ndiko hupatika. Mbinu za ukusanyaji data iliyotumika ni mbinu ya usahili. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kuuliza maswali yaliyoandaliwa kuhusu mtazamo wa walimu katika matumizi ya TEHAMA kutumika kufindishia stadi ya kusoma na ilipobidi aliuliza maswali ya ziada au kutoa ufafanuzi zaidi kwa watoataarifa ili kupata taarifa toshelevu. Hivyo, mtafiti aliweza kupata data toshelevu kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Data za utafiti huu zimechanganuliwa kwa mkabala wa kitaamuli.

## 4.0 Mtazamo wa Walimu Kuhusu Matumizi ya TEHAMA katika Ufundishaji wa Stadi ya Kusoma.

Kuhusu lengo la kudodosa mtazamo wa walimu kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma, kwa upande mmoja, matokeo yanaonesha watoataarifa wakiwa na mitazamo tofauti. Kwa upande mwingine, watoataarifa wanakubaliana na matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2.

Hata hivyo, kuna athari za pande mbili katika utumiaji wa TEHAMA katika mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Zipo athari hasi na athari chanya zinazoambatana na utumiaji wa TEHAMA hasa katika mazingira ya vijijini. Katika vipengele vinavyofuata, athari chanya na hasi zinabainishwa mtawalia.

### 4.1 Hurahisisha Kupata Mbinu Mpya za Ufundishaji

Matumizi ya TEHAMA yana mchango mkubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma kwa wanafunzi wa shule za msingi. Mwalimu anaweza kutumia TEHAMA katika

kubaini mbinu mbalimbali mpya za ufundishaji. Walimu waliosahiliwa walibainisha hili katika maelezo yao kuwa TEHAMA inawasaida kujifunza vitu vipya kutoka kwa walimu walioko maeneo mengine. Mwalimu mmoja miongoni mwa watoataarifa waliohojiwa alikuwa na haya ya kusema:

> TEHAMA inanisaidia kupata mbinu mpya za ufundishaji. Mimi ninatumia simu yangu kupitia makundi ya walimu ya whatsapp na you tube ninaangalia walimu wenzangu wanavyofundisha. Na mimi najifunza kitu kipya, ninaweza kuona wanavyotengenza zana zao na namna wanavyohusiana na watoto. Hivyo, inanisaidia kuboresha mbinu zangu za kila siku na kupata ladha mpya inayosaidia kurahisiha ufundishaji. (Mwalimu 1: Shule A, juni 2024)

Maelezo hayo katika nukuu yanadhihirisha kuwa, matumizi ya TEHAMA yanalenga kutoa usaidizi wa kubaini mbinu mpya za ufundishaji kutoka kwa walimu wengine. Mwalimu anaweza kutumia mitandao ya kijamii au kuingia mkondoni na kupakua video mbalimbali zinazoweza kumsaidia kuboresha ujuzi wake wa ufundishaji. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa TEHAMA inaweza kutumika kama kiunganishi cha wafundishaji kutoka maeneo mbalimbali ulimwenguni. Kupitia matumizi hayo ya TEHAMA ufundishaji wa stadi ya kusoma huweza kurahisishwa kwani walimu huboresha mbinu zao na kujifunza njia bora za kudumisha uhusiano mzuri na wajifunzaji kama ilivyobainishwa na mtoataarifa. Matokeo haya yanaafikiana na yale ya Altun (2015) anaeleza kuwa uhusishaji wa teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji huchochea utayari wa ujifunzaji, hali inayorahisisha kufikiwa kwa lengo la ujifunzaji. Pia, matumizi ya TEHAMA yamekuwa na mchango mkubwa kwa walimu kuboresha mbinu zao za ufundishaji na wanafunzi kufaulu vizuri.

### 4.2 Kupata Zana za Ufudishaji

Matumizi ya TEHAMA yanawezesha kupata zana za ufundishaji wa stadi ya kusoma. Watoataarifa wanaeleza kuwa ufundishaji wa madarasa ya awali huambatana na vitendo zaidi. Hivyo mwalimu lazima atafute zana mbalimbali zitakazomsaidia kurahisisha ufundishaji wa darasa lake. Mathalani mwalimu mmoja alieleza umuhimu wa TEHAMA katika upataji wa zana mpya. Mfano wa 2 unabainisha maelezo yake wakati wa usahili kama ifuatavyo:

> Ni kweli, TEHAMA inamchango mkubwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika mazingira ya shule hakuna mkakati wowote wa matumizi ya TEHAMA lakini mimi binafsi ninatumia simu yangu kudownload nyimbo za watoto ambazo huwa nakwenda kuzifundisha darasani. Kila unapotoka wimbo mpya wa watoto najitahdi kutafuta niwafundishe kwa sababu hunisaidia kuwawezesha kujua kusoma na kutambua matamshi ya sauti au maneno mbalimbali. (Mwalimu 2: Shule B, juni 2024)

Maelezo ya mwalimu katika mfano wa 2 yanadhihirisha umuhimu wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Ni wazi kuwa kupitia TEHAMA ni rahisi kwa mwalimu kupata zana mbalimbali zitakazomsaidia katika kukazia maarifa ya kile alichokifundisha darasani. Pia, ufundishaji kwa kutumia TEHAMA huchochea ushiriki wa watoto katika kipindi, na hivyo kusaidia idadi kubwa ya wanafunzi kujua kusoma kwa urahisi na muda mfupi. Matokeo haya yanafanana na yale yaliyobainishwa na Vicent na Msingwa (2021) kuwa TEHAMA humsaidia mwalimu kwenda na wakati kwa kujifunza zana mbalimbali za kisasa zinazotumika kufundishia. Izingatiwe kwamba TEHAMA inahusisha matumizi ya mbinu tofauti na zile zilizokuwa zikitumika awali. Walimu wote waliosahiliwa wanaitazama TEHAMA kama nyenzo ya upatikanaji wa zana mbalimbali za ufundishaji ikiwa ni pamoja na nyimbo. Hivyo, TEHAMA inadhihirisha kukubalika miongoni mwa wafundishaji wa Kiswahili kama Lg2.

### 4.3 Huchochea Mahudhurio ya Wanafunzi

Wanafunzi wanahitaji kuhudhuria darasani kulingana na siku na muda uliopangwa ili kuendana na malengo tarajali. Ufundishaji wa stadi ya kusoma katika shule nyingi vijijini hukabiliwa na utoro wa wanafunzi wa mara kwa mara. Wataoataarifa saba (7) kati ya kumi (10) waliosahiliwa walieleza kuhusu mchango wa TEHAMA katika kuchochea mahudhurio. Mathalani mwalimu mmoja wakati wa usahili na mtafiti alikuwa na haya ya kusema kuhusu mchango wa TEHAMA katika kuongeza mahudhurio ya wanafunzi:

> Mimi baada ya kugawiwa kishikwambi na serikali niliamua kwenda mjini kutafuta nyimbo za watoto na vipindi mbalimbali vya watoto na kuvipakia katika kishikwambi changu. Nilikuwa na redio ndogo

> nyumbani hivyo niliamua kuja navyo shuleni na kutumia kufundishia. Niligundua kuwa mahudhurio yanaongezeka darasani hata wale wanafunzi ambao walikuwa wanasuasua kuja shuleni walianza kuwa na mahudhurio mazuri. (Mwalimu 1: Shule D, juni 2024)

Maelezo haya yanaonesha kuwa matumizi ya kishikwambi chake darasani kuwaonesha watoto video na nyimbo mbalimbali kumechochea ongezeko la mahudhurio ya wanafunzi darasani hivyo kufikia malengo ya ufundishaji kwa urahisi bila kurudiarudia. Hivyo, matumizi ya TEHAMA katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji unaonekana kukubalika miongoni mwa walimu wa somo la Kiswahili kwa wazawa wanaojifunza Kiswahili kama Lg2. Matokeo haya yanaumgwa mkono na yale yaliyoelezwa na bin Noordan Na Yunus (2022) kuwa matumizi ya TEHAMA huchangia kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi na kukuza mtazamo chanya juu ya somo husika. Hivyo matumizi TEHAMA katika madarasa ya awali wakati wa ufundishaji wa stadi ya kusoma ni kichocheo chaya kwa wanafunzi kuhudhuria, kushiriki katika ujifunzaji na kupata matokeo mazuri baada ya ujifunzaji.

Matokeo ya makala hii yamebaini kuwapo kwa mtazamo hasi kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya Kusoma hasa maeneo ya vijijini kama ilivyo kwa shule za wilayani Lushoto. Watoataarifa waliokuwa na mtazamo tofauti kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma yalijiegemeza katika masuala ya mazingira, uchumi na ujuzi kutetea mawazo yao.

**4.4 Ugumu wa Upatikanaji wa Vifaa vya TEHAMA**

Ufundishaji kwa kutumia TEHAMA huhitaji maandalizi makubwa ili kuweza kufikia lengo. Mazingira ya vijijini yanachangia kukosekana kwa vifaa vinavyohitajika wakati wa ufundishaji. Miongoni mwa watoataarifa walieleza kuwa ufundishaji wa kusoma unahitaji uwapo wa runinga, visimbuzi vilivyolipiwa, kompyuta na mfumo wa mtandao, Kwa sababu ufundishaji wa kusoma huambatana na utoaji wa sauti hivyo ni vizuri kuwapo kwa zana zenye sauti. Mathalani mwalimu mmoja alikuwa na haya ya kusema kuhusu upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA:

> Mazingira ya huku lushoto kupata vifaa kama runinga, visimbuzi, kopmpyuta hata simu nzuri ni gharama sana. Hata hivyo tena mtandao

> wa huku kwetu ni tatizo, jiografia ya huku ni milima sana ni mtando unaoshika vizuri ni mmoja tu nao ni usiku ndio unatulia. Hivyo ni vigumu kusema unaweza kufundisha kwa kutumia vifaa vya TEHAMA kwa mazingira haya. (Mwalimu 2: Shule B, juni 2024)

Maoni ya mtoataarifa yanadhihirisha kuwa ugumu wa utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kusoma unatokana na uhaba wa rasilimali vitu. Taasisi hazina uwezo wa kununua vifaa hivyo kwa ajili ya matumzi ya ufundishaji na ujifunzaji. Hata hivyo, gharama za uendeshaji na upatikanaji wa mfumo wa mtandao ni changamoto kwa maeneo mengi ya Wilaya ya Lushoto. Kutokana na hali hiyo hawaoni kama matumzi ya TEHAMA yana mchango katika ufundishaji wa stadi ya kusoma katika mazingira ya wilaya ya Lushoto. Matokeo kama haya yalibainishwa katika utafiti wa Akintunde na Angulu (2015) walibaini kuwa baadhi ya changamoto za kutumia Teknolojia katika nchi zinazoendelea katika ufundishaji na ujifunzaji ni uchumi mdogo wa kuweza kumudu kununua na kuendesha vifaa hivyo katika mazingira ya shule hali hiyo ina ambatana na uhaba wa umeme katika maeneo ya vijijini.

**4.5 Ukosefu wa Ujuzi wa Kutosha Kuhusu TEHAMA**

Matumzi ya TEHAMA yanahitaji uelewa na ujuzi binafsi wa mtumiaji. Mathalani mwalimu anapaswa kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu TEHAMA, namna sahihi ya kutumia vifaa vya TEHAMA na wakati wa kutumia mbinu hizo za TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Imebainika kuwa walimu wengi hawana ujuzi wa matumzi ya vifaa vya TEHAMA. Mwalimu mmoja alieleza kama ifuatavyo:

> Kwa kweli sina uelewa mpana juu ya matumzi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.  Sina kompyuta na sijui kuitumia. Mimi natumia simu yangu tu, Pia, nayo sijui mambo mengi sana yaliyomo. Nikihitaji kitu nawatumia watoto wangu kukamilisha ninachohitaji. Hivyo sijui chochote kuhusu teknolojia na mambo yake. (Mwalimu 2: Shule E, juni 2024)

Ukichunguza maelezo hayo hapo juu katika mfano wa 3 utabaini kuwa walimu wanakosa ujuzi kuhusu vifaa vya TEHAMA na matumizi yake mbalimbali. Hivyo, kukosekana kwa ujuzi huo

kunasababishwa na kuchelewa kuingia kwa teknolojia nchini na hasa maeneo ya vijijini. Hali hii imesababisha walimu kuendelea kutumia mbinu za kitamaduni katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Mbinu zinazotumiwa ni kama vile kusoma ubaoni, kusoma chati na vitabu vilivyokatika nakala ngumu. Rintaningrum (2023) anaeleza kuwa miongoni mwa sababu za hasi za kutohusisha teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji ni pamoja na umri mkubwa wa walimu unaosababisha kushindwa kwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia. Hali hiyo husababisha walimu kushindwa kujifunza vitu vipya kila mara hata kukosa ujuzi wa kutosha katika kutumia vifaa vya TEHAMA. Aidha, ukosefu wa muda wa kutosha kuhusisha teknolojia katika ufundishaji kwa sababu ya wingi wa vipindi na majukumu ya mwalimu huchangia kupuuza kutafuta ujuzi kuhusu TEHAMA na kisha kuutumia katika kufundishia. Hivyo matokeo yatafiti hizi yanaafiki kuwapo kwa changamoto ya ujuzi wa matumizi ya TEHAMA kwa walimu wa madarasa ya awali.

Mawazo haya ya walimu kuhusu matumzi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma nchini Tanzania hususani wilayani Lushoto yanagonga kengele kuashiria mambo kadhaa muhimu kuhusu nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwanza, matumzi ya TEHAMA katika maeneo ya vijijini hususani wilayani Lushoto yanakabiliwa na changamoto za upatikanaji, umiliki na uendeshaji. Vifaa vya TEHAMA kama vile kompyuta, vishikwambi, projekta na simu janja hupatikana kwa shida na gharama zake sokoni ziko juu. Pia, taasisi za elimu hasa shule za msingi zilizotafitiwa hazina bajeti kwa ajili ya manunuzi ya vifaa hivyo. Vilevile, upatikanaji wa mfumo wa mtandao una changamoto kwa kiwango kikubwa hivyo kupata ugumu wa upakuaji wa vitu mkondoni. Hali hii, husababisha walimu kuendelea kutumia mbinu za kitamaduni katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma.

Pili, ukosefu wa ujuzi wa vifaa vya TEHAMA na programu zake unachingia kuzorota kwa matumizi ya mbinu za kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Data zimeonesha kuwa walimu wengi wanaofundisha madarasa ya awali ambayo ndiyo hujenga msingi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi, hawana ujuzi wa TEHAMA. Hali hii, inasababisha walimu kutumia mbinu zilezile ambazo hutoa matokeo yasiyo bora sana baada ya mwisho wa mwaka, kwani si wanafunzi wote wanamudu stadi ya kusoma.

Tatu, hali ya mazoea huchangia kuhafifisha matumizi ya TEHAMA walimu waliotoa taarifa wanaonesha kuwa hupendelea matumzi ya mbinu za kitamaduni katika ufundishaji wa stadi ya kusoma. Mwanafunzi hufundishwa kusoma herufi zilizoandikwa katika kadi, chati, ubaoni au chini ili kujenga stadi hii muhimu. Matumizi ya mbinu hizi za kitamaduni husababisha kuchelewa kufikia lengo kwani baadhi ya wanafunzi hawavutiwi na matumizi ya mbinu hizi na huchochea utoro kwa kukosekana ubunifu katika ufundishaji.

Nne, matokeo yanaonesha kuwa matumizi ya TEHAMA katika maeneo ya vijijini ni kwa ajili ya kukazia maarifa ya walimu na wanafunzi. Yaani mwalimu hutumia programu za TEHAMA kupakua nyimbo au kujifunza na pia kuona namna walimu wa sehemu tofauti wanavyofundisha stadi hii katika mazingira yao. Hivyo, TEHAMA inatekeleza jukumu hili kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na majukumu mengine ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 5.0 Hitimisho

Kwa ujumla matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma ni ya muhimu sana. Mathalani, ujifunzaji wa stadi ya kusoma kulingana na matokeo ya utafiti huu yanaonesha mchango mkubwa wa TEHAMA kwa walimu wanaofundisha Kiswahili Lg2 kwa Wasambaa wilayani Lushoto. Hata hivyo matumizi ya TEHAMA vijijini katika ufundishaji bado ni wa kiwango kidogo kwa sababu ya changamoto za upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA, uwezo wa uendeshaji wa vifaa hivyo na ukosefu wa ujuzi wa matumizi ya vifaa vya TEHAMA kwa walimu wa madarasa ya awali.

## 6.0 Mapendekezo

Makala haya yanapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu njia bora zitakazowezesha kupenya kwa matumizi ya TEHAMA hasa maeneo ya vijijini katika ufundishaji wa stadi za kusoma.

## Marejeleo

Akintunde, F. A., & Angulu, Y. D. (2015). The use of Information and Communication Technology (ICT) in the teaching and learning of English language in Nigeria. *Journal of Literature, Languages and Linguistics,* 15, 44–50

Altun, M. (2015). The integration of technology into foreign language teaching international. *Journal on New Trends in Education and Their Implications*, 6(1). http://www. ijonte.org/FileUpload/ks63207/File/03a.altun.pdf

Davis, F. (1989). Perceived usefulness, perceived ease of use, and user acceptance of information technology. *MIS Quarterly*, 13, 319-340

Instefjord, E. J., & Munthe, E. (2017). Educating digitally competent teachers: A study of integration of professional digital competence in teacher education. *Teaching and Teacher Education*, 67, 37–45.

Padurean, A., Na Margan, M. (2007). Foreign language teaching via ICT. *Revista de Informatica Sociala*, 12 (2009): 2-7.

Proshkin, V., Glushak, O., Na Mazur, N. (2018). The modern trends in future foreign language teachers` training to ICT usage in their future career. *The Modern Higher Education Review*.2 (2018). DOI:https://doi.org/10.28925/2518-7635.2017.2.15.

Rintaningrum, R. (2023). Technology integration in English language teaching and learning: Benefits and challenges. *Cogent Education*, 10(1), 2164690, DOI: 10.1080/2331186X.2022.2164690